OFISI YA RAIS – TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA

Simu: **0756513626 Mkuu wa shule**

0786377660 Makamu Mkuu wa Shule

0764658855

SHULE YA SEKONDARI ITUNGE,

S. L. P 367,

KYELA.

Kumb. Na. KDC/JI/13/2020. 5/12/2020

NDUGU: ……...,

S. L. P ……..,

KYELA.

YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ITUNGE MWAKA 2021.</u>

1.0. <u>UTANGULIZI.</u>

Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha KWANZA katika shule hii mwaka 2021. Shule ya Sekondari Itunge ipo umbali wa **km 4** Mashariki mwa Mji wa Kyela. Muhula wa kwanza wa masomo unaanza **tarehe 11/01/2021**, unatakiwa kuripoti shuleni **tarehe 07/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni **tarehe 11/01/2021**. Unatakiwa kufika bila kukosa .

2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

2.1. SARE YA SHULE.

(A) WAVULANA.

- Suruali mbili, moja ya **rangi ya Lavender** na nyingine ya **rangi ya Bluu bahari** (Ona kitambaa)isiyo bana chini, Mashati mawili **meupe mikono mifupi.**

(B) WASICHANA.

- Sketi mbili (Ndefu), moja ya **rangi ya Lavender** na nyingine ya **rangi ya Bluu bahari** (Ona kitambaa), Mashati mawili **meupe mikono mifupi.**
- **Hijabu (Kwa Waislamu)** Kitambaa lazima kifanane na rangi ya shati.

WOTE:

(a) Viatu vya ngozi nyeusi, vifungwavyo kwa kamba; Jozi mbili. NI MARUFUKU KUVAA VIATU VYA PLASTIKI (YEBOYEBO).

(b) Soksi nyeupe ndefu (Wasichana) na Nyeusi (Wavulana) (Jozi 2)

(c) Sare za Michezo ni Track Suit rangi ya Blue bahari na viatu vya michezo.

(d) Sweta rangi ya Lavender.

(e) **T – shirt rangi ya maziwa (dark cream) zenye nembo ya shule.** Pia zinapatikana shuleni kwa gharama ya Tshs. 10,000/=

2.2. Daftari **Kumi (10) kaunta quire 3** kwa ajili ya kuandika nukuu za masomo na daftari **Kumi (10) aina ya Msomi** kwa ajili ya mazoezi, Kalamu na Mkebe wa Hisabati.

2.3. Chakula cha mwanafunzi (Wa Kutwa) masomo yanaendelea hadi saa 11:00 jioni, Nauli ya kwenda na kurudi nyumbani pamoja na matibabu.

2.4. Mzazi au Mlezi anapaswa kuhudhuria vikao vyote vya wazazi vinavyoitishwa shuleni kila mhula au dharura.

3.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule **inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978** na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria **Na. 10 ya mwaka 1995**. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Elimu ya Juu, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya Elimu Nchini na Ofisi ya Rais – Tamisemi, Utumishi na Utawala Bora yenye majukumu ya Usimamizi na Uendeshaji Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa Nakala yako mara baada ya kuripoti Shuleni.

(a) Heshima kwa Viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wote, Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation).
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kizingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani.
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
(i) Kutunza mali za Umma.

3.1. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

(a) Wizi.
(b) Uasherati na Ushoga.
(c) Ubakaji.
(d) Ulevi na Matumizi ya Dawa za Kulevya kama vile Bangi, Pombe, Cocaine, Mirungi, Kubeli, Mandrax, Heroin na kadhalika.
(e) Kupigana au Kupiga.
(f) Kuharibu kwa maksudi mali ya Umma.
(g) Kudharau Bendera ya Taifa.
(h) Kuwa Mjamzito/ Kupata Mimba
(i) Kuoa au Kuolewa.
(j) Kutoa Mimba.
(k) Kugoma, Kuchochea na Kuongoza au Kushiriki kuvuruga amani na Usalama wa shule au watu.
(l) Kukataa adhabu kwa maksudi.
(m) Kuwa na Simu ya Mkononi.

4.0. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.

(a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti Shuleni.
(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki migomo, fujo na makosa ya jinai.
(c) Fomu ya Mzazi au Mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa shuleni.

5.0. TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEZO/MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.

……..
B. F. NGOBEI

MKUU WA SHULE.

A.

PRESIDENT'S OFFICE
REGINAONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
KYELA DISTRICT COUNCIL
ITUNGE SECONDARY SCHOOL P.O.BOX 367 KYELA MBEYA

REF NO,MOEVT/S3130

The Medical Officer

: …….

PART A:

RE:EXAMINATION OF MR/MISS……

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time student in this School.The examination should include the following categories

(a) Haemoglobin _____

(b) P.V.Bleeding _____

(c) Sight _____

(d) Blood pressure _____

(e) Urine for Sugar and Pregnancy test _____

(f) Stool for routine examination_____

(g) Athma_____

(h) Skin desease_____

(i) Leprosy_____

(j) Any deformity_____

(k) Epilepsy_____

(l) Pulmonary tuberculosis_____

(m)Neurosis_____

(n) Venereal diseases_____

(o) Other serious diseases _____

PART B.

(To be completed by Government medical officer)

I have examine the above named and consider that he/she physical and mental fit/unfit for full schoolin**.**

Signature……Date……..Designation……..Station…….

C.

FOMU YA MAELEZO YA MZAZI/MLEZI.

JINA LA MZAZI/MLEZI: ……..

Sehemu anakoishi: …… S. L. P ……..... Namba ya simu: ……..

2. SEHEMU YA MZAZI/MLEZI

Mimi ……ninakubali kuwa mtoto wangu (Jina) …….. nitampa mahitaji yote muhimu ya shule **(Ikiwa ni pamoja na chakula cha mchana)** kama yalivyo katika maagizo ya kujiunga na Shule ya Sekondari Itunge. Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mtoto wangu anatimiza wajibu wake kwa Shule na Taifa.

Iwapo nitashindwa au nitapata uhamisho au kubadilisha makazi ni lazima nitaijulisha shule kwa maandishi yaliyothibitishwa.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi: ……

Jina: ……..

Tarehe: …….

JINA LA MWENYEKITI WA SERIKALI YA MTAA/KITONGOJI:……

KITONGOJI/MTAA WA:…… ……S. L. P ……..... Namba ya simu:…

Saini……Tarehe……..Mhuli……